5. The Waves

5. The Waves
Vitabu100Siku100 na Kocha Dr Makirita Amani.

Karibu kwenye muhtasari wa kitabu cha TANO kwenye orodha ya vitabu 100 ninavyosoma kwa siku 100.
THE WAVES ni riwaya iliyoandikwa na Virginia Woolf inayohusu maisha ya marafiki 6 tangu utotoni mpaka uzeeni. Kuna mengi ya kujifunza kutoka kwenye maisha hayo, kuanzia kujua maana ya maisha, jinsi wengine wanavyoathiri maisha yetu, kuchagua kuyaishi maisha yako, kujilinganisha na wengine na kukilabili kifo.

👉Kabla ya jua kuchomoza.
Watoto sita wako kwenye nyumba iliyo ufukweni, ambapo mawimbi ya bahari yanakuja na kuishia kwenye ufukwe.
Walipo ni shule ya awali ambapo wanajifunza na kushirikiana.
Wamewewa zoezi la kusema na kuandika kile wanachoona au kusikia.
Bernard anasema anaona pete ikining'inia juu yake.
Susan anasema anaona ukuta wa njano uliosambaa.
Rhoda anasema anasikia sauti chip krip, chip krip ikienda juu na chini.
Neville anasema anaona tufe linaloning'inia kwenye mlima.
Jinny anasema anaona pindo la bendera, lililofungwa na kamba ya dhahabu.
Louis anasema anasikia kishindo cha mnyama aliyefungwa mguu ila anautikisa.
Bernard, Neville, Jinny na Susan wako kwenye maua pamoja, Louis amejificha hataki wamuone.
Rhoda ameachwa darasani peke yake, wenzake wamejibu maswali na kutoka, yeye hajui cha kuandika.
Baadaye Susan anaonekana amekasirika, anaondoka na kuwaacha Bernard na Neville anakimbia kwenda ufukweni peke yake.
Susan anasema amewaona Louis na Jinny wakibusiana. Bernard anamfuata Susan kwa nyuma, ili amzuie kama anataka kujidhuru.
Susan analalamika kwamba amewaona wawili hao wakipeana mabusu, kitu kinachomuumiza. Anajiambia yeye siyo mzuri kama Jinny.
Bernard anambembeleza na kumwambia asijali, yuko karibu yake kwa sasa.
Susan anasema ndani yake kuna chuki na upendo kwa wakati mmoja.
Louis anakamilisha kazi yake lakini anasema hataikusanya mpaka aangalie kwa Bernard na kunakili maneno yaliyo sahihi, maana yeye ana lafudhi ya Australia.
Rhoda anaamua kujikubali alivyo na kuacha kujilinganisha na Susan na Jinny.

👉Jua limeshachomoza.
Ni siku ya watoto kwenda shule ya bweni kwa mara ya kwanza.
Wavulana wanaenda shule ya wavulana na wasishana shule ya wasichana. Kwa mara ya kwanza marafiki hao sita wanatengana.
Gari imeshafika kuwachukua, wanaagana na familia zao.
Benard anajisikia huzuni, anatamani kulia, lakini anawaona Louis na Neville wakiwa tulivu, anajiambia atakuwa tulivu pia.
Louis anamuona Bernard akiwa tulivu na kujiambia anapaswa awe tulivu na kujiamini kama Bernard.
Wanaingia kwenye gari na kuelekea shuleni, watoto wengine wanajisifia kuhusu wazazi wao, Louis anachagua akae kimya kwa sababu ana lafudhi ya Australia na siyo ya Kiingereza kama wenzake.
Wanafika shule, Louis, Neville na Bernard wanavutiwa sana na mazingira hayo, wanaona ni sehemu ambayo watajifunza mengi.

Susan anaichukia siku ya kwanza ya shule, na kukumbuka vitu vyote alivyoacha nyumbani.
Rhoda anayaona mazingira ya shule kama yatamfanya kuwa mpweke zaidi, kwa sababu huwa hana marafiki wa karibu.
Jinny anawaza vazi alilovaa mwalimu na kuona jinsi lisivyo sawa.
Wanaenda kanisani na kusikiliza mahubiri, Neville anasema maneno matakatifu huwa yanachafuliwa na wale wanaoyasoma.
Ibada inaendelea lakini watoto hao hawaonekani kuifuatilia kwa umakini, kila mmoja anasubiri ibada iishe ili waondoke.
Ibada imeisha, Bernard, Louis na Neville wameenda kukaa uwanjani, Bernard akiwasimulia hadithi ambazo hazikamiliki.
Kwa upande wa mabinti, Susan anaendelea kuhesabu siku ambazo wamekuwa shule, anaziita siku za shule kuwa siku anazozichukia kwenye maisha yake.
Anakumbuka nyumbani, anayakumbuka mawimbi ya bahari na mambo mengine.
Mara zote yuko na Rhoda na Jinny, hapendezwi pia na utaratibu wa kidini wa hapo shuleni.
Susan anajilinganisha na Jinny na kuona Jinny amemzidi urembo. Jinny anajilinganisha na Susan na kuona Susan amemzidi kimichezo.
Rhoda anajidharau kila anapojilinganisha na wenzake wawili, anajiona siyo mrembo, hana akili na pia hayuko vizuri kwenye michezo. Hilo linamfanya azidi kuwa mpweke.
Susan anasema huwa anajenga taswira ya vitu vyote anavyovichukia na kisha kuvizika.
Kwa upande wa wavulana, Louis anaona kundi la wachezaji ambao huwa wanajisifia, anatamani angeweza kujiunga nao ila hawezi. Anatumia muda wake mwingi kujisomea.
Neville pia anaona hawezi kuwa kwenye kundi hilo la wachezaji, lakini pia hapendi kukaa muda mwingi na Louis, kwa sababu Louis anajifunza taratibu. Yeye anaweza kusoma haraka na vizuri kuliko wenzake.
Neville anajiona mpweke, hawezi kukaa na Bernard kwa sababu hadithi zake huwa haziishi na pia hawezi kukaa na Louis kwa sababu ni mtulivu sana. Wengine ni wanamichezo zaidi, hivyo anajikuta muda mwingi yuko peke yake.
Bernard anaona hawezi kujiunga na kundi la wachezaji kwa sababu huwa anachelewa sana, vitu vidogo vidogo huwa vinamsumbua na kujikuta anachelewa. Lakini pia hana utulivu mzuri wa kujifunza kama Louis ila yuko vizuri kwenye hadithi.
Louis pia anajiona mpweke, pamoja na kutumia muda mwingi kusoma, pamoja na kusifiwa na wengine kwenye hilo, bado anaona kuna kitu anakosa kwenye maisha yake.
Siku nane zimebaki kabla ya kufunga shule, Susan anafurahia na kuona siku siyo nyingi atakuwa huru tena, ataondoka kwenye mazingira hayo anayoyachukulia kama gereza.
Hayapendi maisha ya shule ambayo yana ratiba na masharti makali ya kufuata kila siku. Anapenda kuwa nyumbani ambapo yuko huru kuamua afanye nini wakati atakao.
Jinny naye anafurahia siku za mateso zinakaribia kuisha, anapata picha siku akiwa nyumbani, yuko huru, yuko kwenye sherehe na mvulana anamfuata na kumwambia anampenda. Anaona jinsi maisha yake yajayo yatakuwa huru.
Rhoda pia anafurahia siku chache zimebaki kupata muda wa kuwa peke yake. Huwa anapenda muda tulivu wa kuwa peke yake, lakini hapo shuleni hajaupata, kila anapotaka kuwa peke yake kunakuwa na mwingine anayemsumbua au kumuuliza kitu.
Ni siku ya mwisho ya mhula wa mwisho shuleni, Louis anatafakari yale aliyojifunza hapo, mahusiano aliyoyajenga na wanafunzi wengine, anajua maisha yatawatenganisha, lakini watakuwa kitu kimoja.
Bernard anasema hiyo ni siku ya mwisho, ni sherehe ya mwisho kwake kuwa pamoja na wanafunzi wenzake, ambao aliwapenda na hawataonana tena pamoja.
Neville anajiambia ni siku ya mwisho kuwa shuleni, anafikiria jinsi atakavyoachana na wengi aliokuwa nao na maisha mapya anayoyaendea.
Wako kwenye treni kurudi nyumbani, mabinti wanafurahia na kupata picha ya uhuru wanaokwenda kuwa nao.
Louis anafikiria jinsi wenzake wanavyoenda kuendelea na elimu ya chuo kikuu, huku yeye akilazimika

kufanya kazi.
Bernard anafikiria kuhusu kitabu chake anachoandika na kila kinachotokea au anayekutana naye anaandika kwenye kitabu cha kuweka kumbukumbu.
Neville anafikiria maisha ya chuo na kuona hayatakuwa sahihi kwake, angependa sana aanze maisha yake ya kujitegemea.

👉Juma limechomoza.
Mawimbi yanaleta uchafu wa baharini ufukweni.
Ndege wanaimba wakiwa juu na kushuka kwenye uchafu kujipatia chakula.
Bernard yuko chuoni na anayaona maisha ya chuo ni magumu. Ugumu huo unaanzia kwenye kujitambua mwenyewe, anagundua yeye si nafsi moja, bali nafsi nyingi zinazomwakilisha Bernard.
Anafikiria jinsi watu wasivyomwelewa na jinsi wanavyomjadili. Lakini yeye hajali kwa sababu anajua watu hao hawamjui kwa undani.
Bernad anafikiria kuhusu uandishi wake, kwanza anafikiria barua ambayo amepanga mara nyingi kuiandika kwa binti, lakini kila ikifika wakati wa kuandika anaahirisha. Anataka barua hiyo iwe bora na kamilifu kiasi cha msichana huyo kumkubali zaidi. Kadiri anavyotaka iwe kamilifu ndivyo anavyoshindwa kuanza kuiandika.
Pia anafikiria kuhusu riwaya anayopanga kuandika, tayari ana matukio mengi ya kuyaweka kwenye riwaya yake, ila ugumu ni kuweza kukaa chini na kuandika.
Neville pia yuko kwenye mgogoro binafsi, anajiuliza yeye ni nani na hapati jibu.
Anakumbuka vitabu vyote alivyosoma na waandishi ambao ni mashujaa wake, kuna wakati anajiona akiishi kama wao lakini nyakati nyingine anafanya mambo ambayo hayaendani na mashujaa wake.
Anafikiria mashairi ambayo amekuwa akitaka sana kuandika lakini hajaweza kukaa chini na kuandika kwa ukamilifu.
Anajiambia anapaswa kuwa yeye na siyo mtu mwingine yeyote, maana ni vigumu kuwa yeye na kuwa kama wengine kwa wakati mmoja.
Bernard anamfikiria rafiki yake Neville ambaye wamekuwa wakiandikiana barua mara kwa mara.
Anajiuliza iwapo ameweza kupiga hatua kuliko yeye.
Pia anamfikiria Louis ambaye mara zote alikuwa mtu wa kusoma, aliyejiona haendani na wengine.
Bernard anafikiria jinsi marafiki walivyo watu wa kujipima nao.
Louis yuko kwenye mgahawa kupata chakula, anaona watu wakiingia na kutoka, wengine wanapita nje, hakuna utulivu. Anajaribu kutoa kitabu asome, lakini usumbufu uliopo unamfanya ashindwe kusoma.
Bado anajiona mpweke, lafudhi yake inamfanya ashindwe kuongea na wengine maana wanamshangaa.
Anawafikiria Bernard na Neville ambao kwa sasa wanaendelea na masomo, anafikiria kipindi wakiwa pamoja, yeye alionekana mdogo zaidi.
Susan yuko nyumbani, anaamka asubuhi na kusikia sauti za ndege wakiimba, anatoka nje na kuangalia mandhari yanayomzunguka. Anafikiria miaka yote ambayo amekuwa shuleni na sasa yuko nyumbani.
Anajiuliza yeye ni nani ila hapati jibu. Anafikiria siku atakayoolewa na kupata watoto na kuwa na mji wake, akiwa na wasaidizi wa kazi.
Anawafikiria marafiki zake Rhoda na Jinny na kila mara anapata picha ya Louis akimbusu Jinny.
Jinny anajiandaa kwenda kwenye tukio kubwa la maisha yake, ni tukio linalokwenda kumweka huru.
Anaingia kwenye jengo ambalo tukio hilo linafanyika na kisha kuingia kwenye ukumbi, kuna watu wengi na sherehe inaendelea.
Wanaume mbalimbali wanapita karibu yake, wengi anawakataa, anakuja mmoja ambaye anamkubali.
Wanakaa pamoja, anajiona akiwa huru zaidi japo hajamjua mwanaume huyo ni nani.
Bado wako kwenye sherehe hiyo na mara kwa mara hisia zake zinabadilika, akitegemea kupata mwanaume mwingine atakayemkubali zaidi.
Rhoda bado ana hali ya kutokujiamini, hali ya upweke na kushindwa kufanya maamuzi sahihi.

Anajikuta akiwa katikati ya wanaume, akiona yuko kwenye hatari lakini hajui atatokaje.
Anawafikiria marafiki zake Susan na Jinny jinsi walivyo na msimamo, wanaweza kusema ndiyo au hapana, lakini yeye hana msimamo huo.
Anayaona maisha yake yakiwa kwenye hatari ya kuweza kudhuriwa na wengine.

👉Jua linazidi kupanda huku likiangaza kwa mwanga mkali.
Mawimbi ni makubwa baharini, yanayokuja na kuishia ufukweni.
Ndege wanaimba kwa juhudi kubwa, bila kujali wengine wanaimba nini, kwa pamoja mchanganyiko wa sauti zao ni mkubwa.
Bernard yuko kwenye treni akirejea London, anaangalia jinsi mji ulivyo bize na kujiuliza ya nini watu wanajihangaisha hivyo?
Anatafakari jinsi maisha yasivyo na maana, jinsi watu wanajihangaisha kwa mambo yasiyo na umuhimu.
Anayafikiria maisha yake, na kujiona ni mwenye furaha, maana tayari ana mchumba ambaye wanakwenda kuoana.
Anafikiria jinsi atakavyokuwa na watoto ambao nao watapitia yale ambayo ameshapitia mpaka sasa.
Bado swala la kujitambua linamsumbua, anawafikiria Louis na Rhoda na kuona ndiyo watu anaowajua ambao wana utulivu mkubwa kwenye maisha yao, kwa sababu hawahangaiki na watu wengi.
Anawafikiria marafiki wengine, Neville, Susan na Jinny ambao wanakwenda kukutana siku hiyo, anakumbuka jinsi walivyokuwa pamoja utotoni.
Marafiki wote sita wanakutana kwa pamoja. Neville ndiye alikuwa wa kwanza kufika, akafuatia Louis, kisha Susan, Rhoda, Jinny na Bernard alikuwa wa mwisho. Baadaye rafiki waliyesoma naye aitwaye Percival pia aliungana nao, walikuwa wanamuaga maana anaenda India.
Wanakumbushana maisha yao ya utoto mpaka siku wanatengana kwenda shule ya bweni. Tangu hapo hawajawahi kukutana tena pamoja.
Leo wanakubaliana kila mtu aseme siri yake ambayo amekuwa anaificha miaka yote, kwa kuwa wameshakuwa watu wazima hawapaswi kufichana chochote.
Louis anaanza kwa kueleza jinsi ambavyo amekuwa akijiona kama mwanamfalme. Anaeleza jinsi ambavyo amekuwa anawachukia wengine kwa sababu ya lafudhi yake. Anaeleza katika wote ni Susan na Jinny tu ndiyo huwa hajisikii vibaya anapokuwa nao.
Jinny anaeleza jinsi ambavyo amekuwa anapenda kushika umakini wa watu kwa urembo wake. Popote anapoenda huwa anajiandaa na anapoingia lazima kila mtu amwangalie yeye.
Neville anaeleza jinsi anavyoteseka kwenye maisha yake kwa sababu hatosheki. Kila anapopata fedha anazitumia zote, hawezi kuweka akiba na hilo anaona litamtesa maana atalazimika kufanya kazi maisha yake yote.
Rhoda anaeleza jinsi anavyohofia maisha, jinsi ambavyo ana upweke na hawezi kupangilia maisha yake yanavyoenda. Amekuwa akifanya yale wengine wanafanya na amekuwa anakwepa sana kuonekana na wengine.
Susan anaeleza amekuwa akitawaliwa na upendo na chuki kwa wakati wote. Anapenda kile kinachompa utulivu na kuonesha ukuu wake, anachukia kile kinachomsumbua na kuonesha madhaifu yake. Anaeleza amekuwa anamchukia Jinny kwa sababu ni mrembo kuliko yeye.
Bernard anaeleza kwamba kitu asichopenda kabisa kwenye maisha yake ni upweke, akiwa peke yake anachoka na kukosa maana, lakini akiwa na wengine anapata nguvu kubwa. Anawaonea wivu Louis na Rhoda ambao upweke ndiyo nguvu yao, lakini kwake, upweke ni kama kifo.
Wanakubaliana kushirikishana siri zao kunawaleta pamoja zaidi, kunaondoa tofauti zao na kuwafanya kitu kimoja. Upendo ulio baina yao ni mkubwa kuliko chuki ndogo ndogo ambazo zimejengeka tangu utotoni.
Wanaongea kwa muda mrefu, kila mmoja anachangia namna ya kuboresha umoja wao. Wanafikia mwisho na kuagana, wakiahidiana kila mmoja kutunza umoja wao licha ya kuwa na maisha tofauti.

👉Jua limefika kwenye kilele.
Jua ni kali, linatoa mwanga na joto kali.
Ndege waliokuwa wanaimba sasa wametulia.
Mawimbi bado yanaendelea kuja na kuishia ufukweni.
Neville ana masikitiko, amepokea taarifa kwamba Percival amepata ajali na kufariki.
Taarifa hizo zinamfanya aone maisha hayana maana, anashangaa jinsi anavyoona wengine wakiendelea na maisha yao kama hakuna kilichotokea.
Bernard anajikuta njia panda, ana taarifa ya furaha na huzuni kwa wakati mmoja. Mtoto wake amezaliwa na Percival amefariki.
Anaona anahitaji kupata muda wa peke yake na utulivu kutafakari dunia iliyo mbele yake.
Anatembea kuiangalia dunia ambayo Percival hataiona tena.
Anaona jinsi watu wanavyoendelea na maisha yao kama hakuna kilichotokea.
Anajiambia jinsi watu hao wasivyojua walichopoteza, wamempoteza mtu ambaye angeweza kuwa kiongozi wao na mmoja kati ya hao amepoteza mume ambaye angezaa naye watoto.
Bernard anatafakari jinsi Percival amekufa kwa umri mdogo wa miaka 25 wakati angeweza kuishi mpaka miaka 80. Lakini pia anaona kwa miaka hiyo michache Percival ameweza kudhihirisha makubwa. Anajifunza jinsi na yeye anavyoweza kudhihirisha makubwa kwenye maisha yake.
Kifo cha Percival kimemtikisa zaidi Rhoda kuliko wengine wote. Kifo hicho kimemfanya ayatafakari sana maisha yake, kwamba kama kifo kitatokea kwake sasa, ataondoka bila kuacha alama yoyote.
Anatafakari jinsi wengine watakuwa wamepokea kifo hicho, anatembea njiani na kuona wengine wanaendelea na maisha yao.
Anashangazwa, anahuzunishwa mno na kifo hicho na kuona hitaji la kuchukua hatua za tofauti kwenye maisha yake.

👉Jua halipo tena kwenye kilele.
Ndege wameacha kuimba,
Mawimbi yanaendelea kuja ufukweni.
Louis anatafakari jinsi maisha yake ya kila siku yanavyokwenda.
Ratiba zake za kukutana na watu kwa mazungumzo ya kibiashara.
Msaidizi wake kumletea barua mbalimbali anazopaswa kuweka sahihi.
Anajiambia ameshaweka sahihi nyingi za jina lake.
Anaona jinsi wengine wanapambana na maisha yao.
Anamfikiria Percival ambaye amefariki, anamfikiria Susan ambayo tayari ana watoto, anaona maisha yanakwenda kasi sana.
Ana eneo tulivu kwake, ambapo huwa anakaa na kusoma vitabu na pia kutapa nafasi ya kuwaangalia wengine wanaopita njiani.
Susan anambembeleza mtoto ili alale aweze kuendelea na shughuli zake nyingine.
Shughuli ni nyingi na anazifanya tangu jua linachomoza mpaka linazama.
Kubembeleza mtoto alale nayo ni shughuli nyingine inayohitaji uvumilivu.
Anaona jinsi maisha yake yatakuwa hivyo miaka yote, huku akipata watoto zaidi.
Hana tena ule uhuru aliokuwa nao awali, wa kufanya anachotaka, kutembea ufukweni na kukaa bustanini.
Maisha yamebadilika mno, majukumu yake kama mama ni mengi na hayampi muda kabisa.
Jinny anajiambia huu ni wakati wa kukaa pamoja na kuzungumza na mwanaume wa ndoto yake.
Bado hajamjua mwanaume huyo ni nani, lakini yupo tayari wakati wote atakapojitokeza.
Anajikumbusha sifa za wanaume kadhaa ambao anawajua, na wote anaona mapungufu ambayo wanayo.
Anatafakari kwa kina jinsi watu wanavyosumbuka na maisha yao kwenye siku husika, kisha kesho yake zoezi linaanza tena, ni kama mateso yasiyo na mapumziko.
Neville anajiambia hana haja ya kuangalia sana saa. Kwa siku nzima amekuwa na mwanamke ambaye amekuwa anampenda kwa muda mrefu.

Lakini bado anaona kama atampoteza kwenye maisha yake na kurudi kwenye upweke wake.
Anajikumbusha jinsi amekuwa na upweke na kupata kampani kwenye usomaji wa vitabu.
Lakini sasa anahitaji kuyaishi maisha yake halisi na mwanamke wake katika wakati uliopo, bila ya kujali kuhusu muda.

👉Jua limeanza kuzama.
Kuna wingu linalopunguza makali ya jua.
Mawimbi hayana tena nguvu ya kufika ukingoni.
Ndege wanaruka angani, lakini hawaimbi.
Bernard ananyoa ndevu asubuhi ili kwenda kazini, anajishangaa jinsi maisha yake yamekuwa ya mazoea. Kila siku ananyoa ndevu, anaenda kazini, anatekeleza majukumu yake na kurudi nyumbani.
Anajitafakari na kuona amepoteza ujana wake kwa kuishi kwa mazoea, ndoto yake ya uandishi bado hajaanza kuifanyia kazi.
Amekuwa ni rahisi kusumbuliwa na mambo ya nje, hivyo anaona akiwa London hawezi kupata muda tulivu wa kuandika.
Amasafiri kwenda Roma, anajipa siku 10 za utulivu ili aandike. Lakini bado inakuwa vigumu kwake kuandika. Anafikiria maeneo mazuri ambayo hajawahi kuyatembelea kwenye maisha yake.
Pia bado watu wanampa usumbufu, kila anapotaka kukaa aandike, anajitokeza mtu na umakini wake unahamia kwake.
Kwa miaka yote Bernard amekuwa na kijitabu ambacho anakusanya mawazo yake, akiamini siku moja atakaa chini aandike riwaya, lakini hilo halijafanikiwa.
Mawazo ya kuandikia aliyonayo ni mengi, changamoto ni kuweza kukaa chini na kuandika.
Susan yuko kwenye shamba lake na watoto wake, anaangalia hatua kubwa alizopiga katika kuliendeleza shamba hilo.
Lakini anaona maisha yake ndiyo yatakuwa hapo hapo, hayatofautiani sana na miti aliyoipanda.
Anakumbuka kipindi cha utoto, siku aliyochukia sana baada ya kumkuta Louis na Jinny wakibusu.
Anamkumbuka Percival, ambaye anaamini akimpenda sana. Anamkumbuka ba Rhoda pia ambaye hana mambo mengi.
Usiku anafuma, mume wake amelala anaona jinsi maisha yake yatabaki hivyo hivyo, mawimbi yake yakiwa yametulia.
Jinny yuko kwenye stesheni ya treni, anajiangalia kwenye kioo na kujiona umri umeshamuacha, siyo kijana tena.
Anaona pia hajajiandaa kama alivyokuwa anajiandaa siku za nyuma.
Anakubali kwamba muda umemuacha, anakubali kwamba kuna kizazi kipya cha mabinti kinakuja kuchukua nafasi yao.
Lakini bado anamsubiri mwanaume wa maisha yake, hajajua ni nani, anajiambia afanye maandalizi mazuri nyumbani kwake.
Awe na mazingira yatakayofanya mwanaume anayekuja amchague. Anajiambia aweke na vitabu pia, ili hata kama Bernard, Louis au Neville wakija, waone mazingira ni rafiki kwao.
Neville anajiambia hahitaji chumba tena na wala hahitaji ukuta wa kujificha, umri umekwenda na ujana umepita.
Anapita karibu na nyumba ya Jinny na kukuta kijana anagonga mlangoni. Anajiambia hana haja ya kumsumbua, kama atamtaka Jinny atamtafuta kwa wakati mwingine.
Anatafakari jinsi isivyokuwa sahihi kuwahukumu wengine au kuwahubiria nini wanapaswa kufanya.
Anaingia kwenye mgahawa na kukuta kuna vijana wengi wanaendelea na mazungumzo, hawezi kujiunga nao. Anaenda eneo lenye vitabu na kuchukua kitabu asome, lakini umakini wake uko kwenye mazungumzo ya wengine.
Watu wote wanaondoka na anabaki peke yake akiwa mpweke, anawakumbuka Louis ambaye ana chumba cha peke yake ili kupata utulivu na Rhoda ambaye ameenda mbali kabisa ili asisumbuliwe.
Louis anarudi kwenye chumba chake cha utulivu baada ya kutoka kazini.
Anafikiria jinsi kazi yake ilivyo muhimu, jinsi anavyoitekeleza kwa weledi mkubwa na jinsi anavyosifiwa

kwa kazi nzuri.
Mabinti wote wa kazini kwake wanamkubali na kumheshimu sana.
Lakini mwisho wa siku anarudi kwenye upweke wake, anafungua kitabu na kujiambia anasoma shairi moja tu kisha kupumzika.
Anafikiria jinsi maisha yake yamekosa kusudi, anawafikiria Percival na Susan ambao walijua kusudi la maisha yao mapema.
Anamfikiria Rhoda ambaye kwa sasa yuko mbali, ndiye mtu pekee ambaye waliweza kuungana kwneye upweke na ukimya wao, pale wengine walipokuwa wakijichanganya pamoja.
Rhoda yuko milimani peke yake, analaumu jinsi dunia imempotezea muda kwa kumlazimisha awe kama wengine.
Anakumbuka maisha yote aliyoishi tangu akiwa mtoto na shuleni, ya kuiga kile walichokuwa wanafanya wengine.
Anajiona sasa yuko huru kuyaishi maisha yake, pale kwenye mlima alipo ambapo yuko mbali kabisa na wengine.
Anamkumbuka Louis ambaye amemuacha, mtu pekee anayeelewa upweke wanaokuwa nao.

👉Jua linazidi kuzama.
Mwanga wake siyo mkali sana na pia kuna mawingu ya mvua.
Upepo unavuma na mawimbi yanakuja ufukweni, yakiwa yamebeba uchafu mbalimbali.
Ndege wanaendelea kuruka kwenye miti na maua.
Marafiki sita wamekutana tena, sasa wamefika umri wa makamo. Mara ya mwisho kukutana walikuwa vijana.
Bernard anawaambia wenzake ni wakati wa kushirikishana hatua ambazo kila mmoja amepiga, bila ya kuficha hisia zozote.
Bernard anaanza kwa kueleza viwango vya juu vya elimu ambavyo amefikia, ana cheti cha kuonesha hilo.
Anaona wengine wameridhishwa na hilo isipokuwa Susan, ambaye anaonekana mafanikio ya Bernard si kitu kwake.
Bernard anamwambia Susan kwamba maisha yake ya ndoa ni mzigo kwake, yanamfanya awe kama mfungwa na asiwe huru. Wakati yeye anayafurahia maisha ya ndoa na kuwa huru.
Anamwambia hamwelezi hayo ili kumuumiza, bali tu ajione na yeye kuna kitu amefanikiwa kuliko wengine kwenye maisha yake.
Anaeleza kwa walikofikia sasa hawawezi tena kubadili maisha yao, tofauti na walipokutana wakiwa vijana.
Susan anaeleza ni kweli anafanya kazi sana, lakini matunda yake anayaona.
Shamba lake linetunzwa vizuri na mazao ni mengi.
Pia ana maisha tulivu na mume wake, huku vitu vikiwa ni vile vile ila vya uhakika.
Hajasumbuka na kitu chochote kwenye maisha yake.
Rhoda anaelezea jinsi alivyochagua kuishi maisha ya peke yake ili kuepuka usumbufu wa wengine.
Bernard anaelezea jinsi ambavyo ameshindwa kuandika. Kila wakati anakusanya mawazo ya kuandika, lakini hajaweza kukaa chini na kuandika.
Anamsifia Louis ambaye anajua kwa kuwa ana chumba cha peke yake ba utulivu, atakuwa ameshaandika kwa kiasi kikubwa.
Louis anasema kwamba japokuwa amekuwa anatafuta sana utulivu, bado usumbufu umekuwa unamuingilia na kukatisha yale anayokuwa amepanga kufanya.
Anawashirikisha mafanikio makubwa aliyopata kupitia kazi yake.
Lakini kwenye uandishi, bado hajafanikiwa kufika mbali.
Anaeleza jinsi anavyothamini urafiki wao huo, yupo tayari kuulinda hata kwa kifo, japo anapenda zaidi kuwa peke yake.
Jinny anaeleza jinsi maisha yake amekuwa akiyaendesha kwa urembo wake. Amekuwa akitumia muda mwingi kujiandaa vyema na amekuwa akiteka umakini wa wengi.

Hajawahi kuwa kwenye hali ya upweke kwa kukosa wa kuwa naye.
Ila sasa umri unamtupa mkono na anaona hilo halitaweza kuendelea.
Bernard anasema wamekuwa na wakati mzuri pamoja na kila mtu amefanikiwa kwa namna yake, licha ya changamoto mbalimbali, kila mtu kuna hatua amepiga katika kuyaishi maisha yake kwa namna anavyotaka mwenyewe.
Wanaondoka wawili wawili, Bernard na Susan, Neville na Jinny, Louis na Rhoda.
Wanapata muda wa kuwa pamoja, wakizunguka ufukweni na kukumbushana jinsi ambavyo wamekuwa wanapendana kwa muda mrefu.
Wanaona jinsi mji unavyopumzika, watu wakienda kulala na kujua kesho wataamka na kuendelea na maisha kama ulivyo kwenye siku nyingine za maisha yao.

👉Jua limezama kabisa.
Kuna mwanga hafifu ambao unaleta vivuli vya vitu.
Sauti za ndege wanaotafuta makazi yao zinasikika.
Mawimbi yanaendelea kuja ufukweni.
Bernard anasema maana ya maisha ya mtu huwezi kuijua kwa kumuangalia.
Ni mpaka yeye mwenyewe akupe hadithi ya maisha yake, hadithi inayohusisha mambo mengi, kuanzia utoto, masomo, ndoa, kazi n.k.
Kwa bahati mbaya sana, wengi wamekuwa wanaremba hadithi za maisha yao na hivyo kuwa tofauti na uhalisia.
Anaelezea hadithi yoyote ya maisha yenye mambo mazuri tu siyo ya kweli. Kila mtu anapitia magumu na mabaya kwenye maisha yake. Ili ujue maana ya maisha yake lazima ujue yote hayo.
Bernard anakumbuka matukio ya shule ya awali, siku aliyoadhibiwa kwa kukosa utulivu, siku aliyomuona Susan akiondoka kwa hasira na kwenda kumbembeleza. Anakumbuka matukio yote yanayowahusisha wenzake watano.
Anakumbuka matukio ya shule ya sekondari, hasa kipindi cha dini ambacho hakikupenda kutokana na mwalimu aliyefundisha.
Anamkumbuka Percival, ambaye alionesha uwezo mkubwa tangu akiwa shuleni, lakini alifariki mapema, anaona jinsi dunia imekosa mengi kwa kufariki kwake.
Anamkumbuka Louis ambaye muda mwingi alikuwa peke yake na alionekana uwezo wake ni wa chini kuliko wengine. Aliona kwamba anamuonea wivu kwa kuwa yeye Bernard aliweza kuandika vizuri zaidi.
Anamkumbuka Neville ambaye alionekana kutokujali na alitumia muda wake mwingi kusoma vitabu, hasa vya lugha ya Kilatini. Neville alimsaidia sana kwenye lugha hiyo.
Anakumbuka matukio mengi ya maisha yake ambayo yamechangia kuwa vile alivyo sasa.
Bernard anasema pamoja na yote, maisha yanavumilika na mtu unaweza kuyafurahia. Jumanne inafuata baada ya jumatatu, maumivu yanakuwa sehemu ya ukuaji, muda unakwenda kasi na mambo yanajirudia.
Bernard anasema baadhi ya watu huenda kwa wachungaji wanapokuwa na msongo, wengine husoma mashairi, lakini yeye huenda kwa marafiki zake, kwani kupitia wao anapata njia ya kukabiliana na chochote.
Marafiki zake wote wameshakufa, ni yeye tu aliyebaki hai lakini kila akikumbuka maisha yao, kuna mengi ya kujifunza na kumwezesha kukabiliana na chochote.
Bernad anajiambia yeye siyo mtu mmoja, bali ni mchanganyiko wa watu wengi, kila rafiki yake akiwa sehemu ya watu hao.
Anafikiria jinsi ambavyo amekuwa akikusanya mawazo ya kuandika miaka yote, lakini hajawahi kuandika.
Ni mzee sasa, ameshakata tamaa na haoni tena cha tofauti anachoweza kufanya.
Bernad anamkabili adui mkuu wa maisha ambaye ni kifo, anawafikiria marafiki zake wote ambao wameshakufa na hilo linamfanya awe tayari kukikubali kifo.

Muhtasari huu umeandaliwa na Kocha Dr Makirita Amani,
www.t.me/somavitabutanzania